# KISWAHILI KARATASI YA PILI

# ANSWERS

# KCSE 2010

Coordinated by KENPRO, Macjo Arcade, 4th Floor, Suite 15E, Off Magadi Road, Ongata Rongai |Tel: +254202319748 | E-mail: infosnkenya@gmail.com | Website: www.schoolsnetkenya.com/

## 30.2.2 Kiswahili Karatasi ya 2 (102/2) Mwongozo wa Kusahihishia

1. (a) Kukichungua au kukiangia kipindi cha mahusiano yenyewe.

   (b) Kuwa utakuwa uhusiano wa kudumu/utakuwa uhusiano wa muda mrefu.

   (c) Huwezesha watu au jamaa walio mbali kuwasiliana/simu au mtandao huwa chanzo au nyenzo muhimu ya kudumisha uhusiano.

   (d) Mabadiliko ya mara kwa mara/kuwepo kwa ubinafsi mwingi.

   - Uhamaji wa watu kutoka viambo/mitaa yao
   - Ufutwaji wa watu kazini na kwa hivyo kutengana na wenzao.
   - Ubadilishaji wa kazi.
   - Kutotegemeka kwa kazi zenyewe.
   - Nguvu na kani za kiuchumi ni nyingi.
   - Mifumo ya kisiasa huweza kuathiri maisha.

   (e) Uhusiano wa chembechembe/mtu hujihusisha na chembe ndogo ya mwenzake. Mahusiano yanapasa kutawaliwa na hisia za utu, undani – yaani mahusiano yanayogusa nafsi zetu,ya dhati, ya kuwajibika kwa wenzetu na nchi yetu.

   (f) (i) Inapingana;
   (ii) yamejaa/yametawaliwa na
   (iii) vinyume

2. (a)
   - Maarifa huyadhibiti maisha ya binadamu
   -Maarifa ni nguvu muhimu maishani
   -Utajiri na maendeleo hutegemea maarifa
   -Maarifa hayana upinzani
   -Maarifa hayamalizwi kwa kutumiwa na watu tofauti
   -Maarifa hayagusiki

   zozote 4 x 1=4
   ut – 1

   (b)
   -Maarifa huingiliana na maarifa mengine
   -Huweza kuchukuliwa kutoka sehemu moja hadi nyingine
   -Huweza kuwasilishwa kwa njia ya ishara
   -Yana sifa ya uhusianaji
   -Huweza kuhifadhiwa katika nafasi ndogo
   -Hayawezi kuzuiliwa yasisambae. zozote 4 x 2=8
   Ut -2

   (a) au, oa, au (alama 1)

   (b) (i) Barabara – sawasawa
   Bara bara – njia (alama 2)

   (c) Abiria walisafiri kwa ndege (alama 1)

   (d) (i) Mkongwe – Kivumishi jina (alama 2)
   (ii) Hodari – Kivumishi cha sifa (alama 2)

   (e) Ungeacha masomo, ungetaabika vile. (alama 1)

   (f) Mifano ya sentensi:
   (i) Kenya ilinyakua nishani **lukuki**
   (ii) Ali alikariri mashairi **kimanju** (alama 2)

   (g) -Shamirisho – kazi
   -Chagizo – haraka ipasavyo (alama 2)

(h) -Amletee mbuzi mnyama
-Amletee mbuzi kifaa cha kukunia nazi (alama 2)

(i) Mfano wa sentensi: **U**singizi **u**memlemea sana (alama 2)

(j) Mwanamazingira alituhimiza kuungana mikono wakubwa kwa wadogo, wanaume kwa wanawake kusafisha mito yetu ambayo ilikuwa imechafuka sana. (alama 3)

3. (k) (i) Mistari:
KN(N) + KT(T+N)

( ii) Mishale:
S ——————▶ KN + KT
KN – N
N – Amina, Mustafa
KT –TN + N
T – huimba
N – taarabu

*Sahihisha aina moja pekee ya uchanganuzi. (alama 4)

(I) (i) **Ku** katika sikumwelewa ni kiwakilishi cha wakati katika hali kanushi.
(ii) **Ku** Katika **kuwatunza** ni ya ngeli ya kitenzi – nomino (alama 2)

(m) Mfano wa sentensi: Chakula kimeliwa (alama 2)

(n) (i) Angetaka ni kitenzi kisaidizi ambacho kimebeba dhana ya wakati.
(ii) Kupalilia ni kitenzi kikuu au halisi ambacho kinaendeleza maana kuu ya sentensi. (hoja 2 x 2=alama 4)

(o) t- Chepesi (sighuna)
d- nzito (ghuna)
Kutaja 2 x 1 =2
Tofauti 2 x 1 =2 (jumla=alama 4)

(p) (i) (a) Kuonyesha/kuashiria kutua au kupumzika katika sentensi ndefu.
(b) Kuunga sentensi mbili au vishazi viwili vinavyoweza kusimama huru.
(c) Kabla ya maneno ya kutolea ufafanuzi
(d) Katika sentensi ambapo kuna orodha hiyo
Tanb: Anaweza kutoa mifano au maelezo tu. (alama 3)

(ii) Herufi kubwa:
1) Mwanzoni mwa sentensi
2) Kuandika majina maalum/nomino za pekee
3) Kuandika majina ya siku, mwezi au mwaka
4) Kuandika anwani ya kitabu/makala/kuanzia kila neno muhimu. Katika anwani k.m Mayai Waziri …
5) Kuandika vifupi vya maneno na akronimu k.m S.L.P, UKIMWI

**yoyote 1x 1=1**

(iii) Kishangao: (alama ya hisi)
1) Kuonyesha hisia (furaha, huzuni, mshtuko)
2) Kuonyesha amri au sharuti. **yoyote 1 x 1=1**

4. **ISIMUJAMII**

(a) Sajili ya hospitalini/sajili ya matibabu. Mazungumzo yanayopatikana katika muktadha wa hospitali.

(b) (i) Matumizi ya msamiati maalum – magonjwa, mkamba, maradhi, pimajoto, udodosi n.k.
(ii) Mwelekeo wa kuchanganya ndimi na kuhamisha ndimi.
(iii) Sifa ya kuwarejelea wanaohusika kwa kutaja vyeo vyao … Dkt… Muuguzi… au mgonjwa badala ya kutaja jina/majina yao.
( iv) Kuchanganya lugha na ishara au alama, kwa mfano 1 x 3 (tembe moja mara tatu).

(v) Matumizi ya lugha ya kilatini – hasa wakati wa kurejelea taaluma au mapana maalum.

(vi) Matumizi ya vifupisho kwa mapana kwa mfano CD4, TB, VVC

(vii) Kuwepo kwa msimbo maalum/mwelekeo wa kutumia msamiati au maelezo tofauti na lugha ya kawaida. Kwa mfano mgonjwa huyu afanyiwe 'Elisa test' badala ya mgonjwa huyu apimwe maradhi ya ukimwi kwa kutumia kipimo cha Elisa."